

SWAHILI FORUM 22 (2015): 1-19

TASWIRA ZA NDEGE

KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

AHMAD KIPACHA

Sifa mojawapo ya umahiri wa Shaaban Robert ni namna anavyounda katika maandiko yake taswira mbalimbali za viumbe wenye mbawa kama vile ndege wakubwa ‘wahamao’, ndege waimba, malaika na wadudu, kwa minajili ya kuwajengea wasomaji wake motifu za upazo, ukwezi na safari. Wahakiki mbalimbali wameusadifu ufundi wake wa kuunda taswira za kisitiari na ishara katika fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Hata hivyo, uchunguzi wa hakiki zao kifani una mapengo haswa katika kubaini taswira na ishara zitokanazo na kiumbe ndege. Makala haya yanachambua namna Robert anavyotanabaisha kanikinzani mbalimbali kupitia taswira za ndege. Robert amefuzu kuchota taswira za ndege kutoka katika mitholojia ya ndege ya wanajamii wake ili kuwagusa kisitiari wasomaji wake.

One of the key aspects of Shaaban Robert’s artistic techniques is his remarkable molding of winged creature images in the form of extraordinary migratory birds, songbirds, angels and winged termites to infuse the motif of ascendance, progress and journey. So far critics of Robert’s works have given this significant artistic tool a very low prominence in spite of its recurrence in his writings. This paper argues that Robert devulges two opposing forces through scary bird imagery. Robert successfully displays his creative artistry by supplanting the bird mythology drawn from the reservoir of folkloric knowledge of his people to appeal metaphorically to his readers’ senses.

Utangulizi

Si rahisi kudurusu kurasa kadhaa katika maandiko ya Shaaban Robert¹ bila ya kukutana na uundwaji wa taswira zitokanazo na viumbe wenye mbawa kama ndege, wadudu, na malaika ambao amewatumia kujenga motifu za upazo, ukwezi na safari. Wahakiki wamemsadifu Shaaban Robert kwa ustadi wa juu katika ujenzi wa ishara na taswira mbalimbali. (Sengo 1975, Gibbe 1980, Senkoro 1988, Oriedo 2000, Khamis 2001, Khatib 2011, Ponera 2014 na Thomas 2015) Senkoro amempamba Shaaban Robert kama fundi “wa kutumia tamathali za semi hasa za *sitiari*, tashbiha, matumizi mazuri ya sanaa ya lugha pamoja na ya ishara na taswira” kiasi cha kupewa cheo cha “ushaha wa malenga.” (1988: 137) Gibbe naye kamsifu juu ya ustadi wake wa “kuya-fanya mawazo yaguse zaidi kutokana na matumizi mema ya picha.” (1980: 78) Hata hivyo, Oriedo katika tasnifu yake ya uzamivu ihusuyo “Fani Katika Riwaya za Shaaban Robert: *Kusadikika, Utubora Mkulima na Siku ya Watenzi Wote: Uhakiki wa Kiurasmi*”, haridhishwi na idadi ya hakiki za vipengele vya fani katika nathari za Shaaban Robert, haswa vipengele vya *taswira*, tataruki, monolojia, dayolojia, balagha, semi za kitamathali na takriri. (2000: iii)

¹ Shaaban Robert aliyejukwa mshairi na mtunzi wa nathari katika Fasihi ya Kiswahili, na kuishi kati ya 1909 na 1962 nchini Tanganyika, katika nyakati za utawala wa Kijerumani, Kiingereza na mwanzoni mwa madaraka ya wenyeji Waafrika chini ya Julius Nyerere, huhesabika kuwa ni mionganoni mwa waandishi bora ulimwenguni kiasi cha kulinganishwa na “Shakespeare, Pushkin, Goethe na Bunyan. (Harries 1966, 1975, Ndulute 1987 na Zhukov 1998)

AHMAD KIPACHA

Mchango wa makala haya ni kujadili taswira za ndege, na mbawa zake katika "dafina" za Robert. Tunajenga hoja kuwa Robert anakusudia kuwazindua wasomaji wake kutoka katika lepe la kudorora na kukandamizwa, kupitia taswira mbalimbali zinazonasibishwa na kiumbe ndege. Kwa ujumla, Robert anawarejelea viumbe mbawa katika makundi mbalimbali: "ndege na wadudu asilia" (*vitwitwi, membe, tai, mangera, kurumbizi, mwewe, kumbikumbi, nyuki wavivu na nyuki wa asali*); "ndege–ulaya" (*eropleni*) na viumbe-jini (*Malaika, Shetani na Mrefu* (Jini-mtu))². Matumizi ya taswira za ndege anazozitumia Robert si ngeni kwa wanajamii wenzake waliomzunguka. Kwa mujibu wa Senkoro "taswira haina budi kuchotwa kutoka katika mazingira na maisha ambayo wasikilizaji au wasomaji... wameyazoea na wameyaishi." (1988: 23) Na Khamis pia anaona ipo haja ya taswira kuibuliwa kutoka katika mazingira yanayomzunguka mwandishi (2004: 31). Katika ulinganishaji wa ustadi wa ushairi wa Shaaban Robert na Muyaka bin Haji, Khatib anajenga rai sambamba na Khamis na Senkoro kuwa:

Picha katika shairi fulani huibuka kutokana na mazingira na maumbile ya jamii fulani ambamo mshairi huchota vitajwa vya viumbe kama wadudu, wanyama, matunda, ndege, madini na hata vito vya thamani kama vitomeo vya utungo fulani wa ushairi unaojitofautisha na mashairi ya jamii nyingine. (2011: 29)

Uteuzi wa taswira za ndege ni sehemu ya sanaa,³ lugha za kifasihi (ngano, visaasili, methali, ushairi, nyimbo, majigambo), kibalagha (hotuba), na hata lugha za kawaida.

Ikumbukwe kwamba Robert alishawaonya wasomaji wake kupitia mhusika wake aitwaye *Mrefu* katika *Adili na Nduguze*⁴, kuwa "Neno takatifu gumu kufahamika lakini tija kwa wajisumbuao kulifasiri. Kila msaada nitakupa wa kulitafsiri." (Robert 1980: 29)⁵ Na katika *Kielezo*

² Khatib amegawa makundi mbalimbali ya vyanzo vya sitiari kama vile sitiari za *kizuojoja* (viumbe hai i.e ndege, wadudu) na sitiari za *kiteolojia* (Malaika, Mungu, Majini, Shetani). (2011: 192) Makundi mengine aliopendekeza ni *astrolojia* (sayari, wingu na nyota), *jiolojia* (fedha, shaba, lulu), na *kawaida* (mlango, kitambi). Hii inathibitisha namna kategoria ya sitiari ilivyo pana na changamani.

³ Sanamu maarufu ya picha ya ndege ya *Sankofa* ambapo ndege anapaa huku kichwa chake kikiangalia nyuma imenasibishwa na methali ya Kiakan "Se wo were fi na wosankofa a yenkyi," ikimaanisha "si vibaya kuangalia nyuma kurejelea kile ulichosahau." (Seeman 2010) Na ile ya *Nnomaa mmieni* ambapo ndege wawili wanaangaliana uso kwa uso imebeba ujumbe wa kuishi kwa kuelewana baina ya pande mbili zinazokinzana kama vile maisha na kifo; au ujana na uzee. (Asante na wenziwe 2015: 7)

⁴ Hii ni riwaya inayoelezea kisa cha mhusika mkuu Adili na ndugu zake kugeuka manyani kwa sababu ya inda, husuda na tamaa. Riwaya inabeba ujumbe wa kusameheana na kuwa na bidii katika maisha. Adili anapambwa na sifa za uvumilivu, ugunduzi na udadisi kimaisha. Robert anamatumia Adili kuonesha haja ya kukwea hadhi kielimu na kutumia maarifa kujilettea ustawi wako binafsi na wanajamii wenzako.

⁵ Mbinu ya kuwaonya wasomaji juu ya mafumbo ndani ya kazi zao (haswa kwa kutumia taswira za ndege) haitumiki kwa Robert pekee. Shani Kitogo (2005: 32) katika Kija: *Chungu cha Mwana Mwari wa Giningi* anawakejeli wasomaji wake waziwazi "fumbo mfumbie mjinga mwerevu atalitambua". Tamthilia yake imejaa taswira za ndege zilizojificha (manyoya, bundi, popo, kunguru, tausi, njiwa, tundu la ndege na hata kumbikumbi). Kwa upande wa Fumo Lyongo naye hakusita kuwfumbia maadui zake aliowaita nyoka na yeze kujinasibu na sifa za makozi (mwewe), akijua fika mama yake pekee ndiye atakayemudu kulifumbua fumbo hilo:

Muinga hayalimka

TASWIRA ZA NDEGE KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

*cha Fasili*⁶ anabaini lengo na mbinu za uandishi wake kuwa ni “kusema fikira” (zake) na kuwaacha wasomaji waamue.⁷ Anasisitiza msimamo huo katika *Kielezo cha Insha*⁸ kuwa “Sitakuwa mwamuzi wa kazi zangu.” (Robert 1954: 80) Wasomaji wanawajibika kufumbua mafumbo yake, ikiwemo taswira za ndege, aliyoaficha katika kile akiitacho kama “kifingirisha kipopo” cha fikira kubwa.” (Robert 1991c: 43) Ili kukifumbua “kipopo” hicho, dhana na vigezo vya taswira za kisitiari katika §2 zatabainishwa. Sehemu ya §3 itajadili ujenzi wa motifu za “upazo” na “ukwezi”. Makala yatajenga hoja kuwa taswira za ndege za Robert ni sehemu ya msuko wake wa sitiari changamani ya “maisha ni safari” katika §4. Makala yatahitimishwa katika §5.

Dhana na Vigezo vya Taswira za Kisitiari

Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 225) na kama alivyonukuliwa na Mnenuka (2010: 70), taswira ni dhana itumiwayo “kuelezea neno, kirai au maelezo yanayounda picha fulani katika akili ya msomaji” wa kazi ya fasihi. Fasiri hiyo ni sawa na ile ya Cuddon (1991: 442-443) iliyonukuliwa na Khamis (2004: 31).¹⁰

Miongoni mwa sifa mbalimbali za taswira ni kwamba zinaweza kuundwa na lugha ya kawaida au ya kitamathali, kujitokeza katika umbo sahili au changamani, kuwepo kwa taswira nyoronyoro au nzito; na zile za asili au za kukopwa (Khamis, keshatajwa: 32). Mnenuka (keshatajwa: 70)

mle tupa na kupika
makozi yakanuika
nyoka hawatajaliya (Mulokozi 1999: 39)

Sifa ya mfalme Somtsweani, katika majigambo ya Kizulu ni ya ndege “kozi” mwenye makucha makali: “Ukhozi lwakith lumezipho.” (Masango 1996: 100) Na katika utenzi wa Hewani Mwana Hewani: Tenzi za Zaynab Himid Mohamed (Yahya Othman na Yahya Abdulhakim 2004: 16) fumbo la njija kuimba wimbo na kutaga mayai mlangoni mwa pango alipojificha mtume Muhammad na sahaba Abubakar walipotoroka Maka, lilishindwa kuteguliwa na mabedui:

Wakaa kwa kitambo
Njiwa wakaimba nyimbo
Akautia urembo
Buibui Mlangoni

⁶ Hii ni diwani ya mashairi ambapo ndani yake Shaaban Robert (1973) anamdokezea msomaji fikra zake na namna ya kuyachanganua mashairi yake.

⁷ Je, huku ni kubadilika kwa msimamo wa Robert? Tunaelezwa katika Senkoro (1988: 128) kuwa katika *Kielezo cha Fasili* alifasili mashairi yake mwenyewe, akayapa maana alizokusudia alipoyaandika. Kwa maoni ya Senkoro, hali hiyo ni “kumbana msomaji au mhakiki wa mashairi kwa kutoachiwa uhuru wa kutoa maana na tafsiri imjiayo mawazoni mwake”, ni sawa na kukatwa “mabawa”.

⁸ Hii ni nathari ya Shaaban Robert (1954) yenyé kulenga stadi ya uandishi wa insha kwa wanafunzi kinadharia na mifano. Mawazo yaliyomo katika insha zake yanaakisi mawazo na mišimamo yake ya kimaisha.

⁹ Kamusi ya Kiswahili –Kiingereza ya TUKE (2001) inafasiri “kipopo nm [ki-] “part of the brain where thinking takes place” (mahali katika ubongo panapohusika na kufikiri).

¹⁰ “The use of language to represent object, feelings, thoughts, idea, states of mind and sensory or extrasensory experience” (matumizi ya lugha kuwakilisha kitu, hisia, fikra, dhana, hali ya kifikra na uzoefu wa kifahiwa au kifahiwa ziada).

AHMAD KIPACHA

anabaini vigezo vinne vyatasmira kwamba (i) “Hazihitaji ufanuzi kwa kuwa zinajulikana” (ii) “Huibua hisia za msomaji/msikilizaji” (iii) “Hudokeza mtazamo wa jamii nzima” (iv) “Kila jamii huwa na ishara mbalimbali.”

Kwa mujibu wa kigezo cha kwanza na cha pili cha taswira, maneno au sentensi hazihitaji ufanuzi pale zinapotumiwa na huibua hisia zinapotumika. Waswahili wamejiundia taswira mbalimbali kama vile “ota mbawa”, usomaji wa “kikasuku”, “ukinda”, mapenzi ya “njiwa”, uzuri wa “tausi”, usaliti wa “popo”, ukipanga, “kijogoo” cha mtaa, ukatili wa “tai”, sauti ya “bundi” na hata uoga wa “kunguru” ambayo ni misemo inayoibua hisia mbalimbali. Na katika mfumo tambuzi au maarifa ya Waswahili, ndege kama bundi husababisha huzuni anaposikika lakini dudumizi huchukuliwa kuwa ni kiashirio cha mvua.¹¹ Huhitajiki kutolea maelezo pale unapotumia semi hizo katika mazungumzo au maandiko. Tayari maana zake zinakuwa zimekwisha jengeta mionganoni mwa wazungumzaji.

Kigezo cha tatu kinaleza kuwa taswira hudokeza mtazamo wa jamii nzima. Uthibitisho wa kigezo hiki unaweza kufafanuliwa vizuri zaidi kwa njia ya semi zenye taswira za ndege kama vile “Kunguru mwoga hukimbiza *ubawa wake*”, “*Bawa la kuku halimwui mwanawewe*” au “*Kipungu huenda mbio* lakini hafiki *mbinguni*”. Katika semi hizo kuna taswira za ndege watatu wanaowakilisha uoga, ulezi na majigambo ya wanadamu. Ingawaje ndege wote watatu wana “mbawa”, uwezo wa urukaji na melodi ya sauti zao hutofautiana na hutafsiriwa tofauti na wanajamii ya Waswahili. Katika jamii ya Waswahili, alikokulia Robert, mbawa si miliki ya viumbi hai pekee. Dhana dhahania zaweza kuoteshwa mbawa. Usemi wa “*Utajiri una mbawa, huruka kama ndege*” (Mulokozi & Kitogo 2007: 68) hujenga picha ya ukwasi kugeuka ukata. “*Mshale usio ngoya hauwendi mbali*” (Mulokozi & Kitogo 2007: 45) hapa mshale unavalishwa “ngoya” kama ndege kuashiria mwendo wa kasi. Mionganoni mwa nyimbo na michezo ya watoto wa Uswahilini huwaomba ndege aina ya *yangeyange* kuwapa kucha nyeupe. Huko makondeni wakulima huwavurumusha ndege waharibifu kwa mawe kwa kutumia “*kumbweye*.¹²”

Kigezo cha nne cha “Kila jamii huwa na ishara mbalimbali” kinapata ufanuzi mzuri kuitia taswira ya ndege *kunguru* (Khamis 2004: 31). Taswira ya *kunguru* huashiria mwanamke maluuni katika nyimbo za taarabu za Zanzibar. Katika tamthilia ya Kitogo (2005: 11) ya *Kija: Chungu cha Mwana Mwari wa Giningi* yenye mandhari ya kisiwa cha Pemba, Muhadi, mmoja wa watusika, anamsasambua mwanamke mwenzie kwa saguo la “Mwanamke konokono sio wewe *kunguru!*” Na mshairi maarufu wa Zanzibar aitwaye Mohamed Ahmed amenukuliwa katika

¹¹ Angalia Mlingwa na Kiango (2006: xvi) wanapozungumzia imani za Waswahili juu ya aina mbalimbali za ndege.

¹² Wasegeju ambao ni watani wa Waswahili katika mji wa Tanga, hukejeliwa ushupavu wao kwa methali ya “Msegeju kumbwewe ya mawe mawili” (Mulokozi & Kitogo 2007: 44). Angalia Kipacha (2015: 210-211) kwa ufanuzi zaidi wa methali hii.

TASWIRA ZA NDEGE KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

shairi lake la “Kunguru” akimdhalilisha mwanamke kwa sifa hasi za kutopendeka, kutofugika, laghai, mwenye tamaa, mwizi na mwoga:

Kunguru ndege laghai, ana tabu kumnasa,
Kama yeye hatokei, mwenye hila na mikasa,
Japo ukifanya rai, weka mbele kumkosa. (Khatib 2011: 206)

Kiashirio cha *kunguru* kama mwanamke maluuni hakionekani katika kazi za bara ikiwemo za Robert. Pengine sababu kuu ni kuchelewa kuhamia kwa kunguru pande za Mrima kutokea Zanzibar walipopandikizwa.¹³ Ranne (2010: 60) amepambanua juu ya taswira za kukopwa kutoka katika maandiko au jamii tofauti. Taswira za utakatifu wa ndege kama alivyo *hudihudi* wa Mfalme Suleiman na *njiwa* aliye ishara ya “roho mtakatifu” pamoja na miujiza ya viumbe mbawa kama *malaika, buraq, shetani*, na *majini* kama zilivyorithiwa kutoka katika maandiko na masimulizi ya Korani na Biblia.

Kimuundo taswira ndani yake ina kipengele cha sitiari ambacho Wamitila (2003: 202) anakifasiri kuwa ni “mbinu ya ulinganishi wa vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia au kimaumbile”. Matumizi ya taswira za ndege katika fasihi na balagha ni mbinu kongwe ya kitamathali inayotumika kisitiari kusawiri mahusiano ya walimwengu kwa walimwengu, Mungu na wanadamu na mazingira na walimwengu. Wanadamu humchukulia ndege kuwa ni mfano wa kiumbe huru, aishiye kwa raha na mwenye kufanya atakalo na kwenda atakako. (Lutwark 1917, Armstrong 1958, Rowland 1978, González 2000 na Moreman 2014)

Mbali ya Robert, waandishi mbalimbali wa Fasihi ya Kiswahili na Wasanii wametumia na wanaendeleza mbinu ya taswira za ndege katika kazi zao ili kufikisha ujumbe waliokusudia. Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti wa Masango (1996) kumekuwepo na majigambo ya kale (na ya sasa pia) ya Wazulu, maalumu kwa ajili ya kuwapamba wafalme wa Kizulu yajulikanayo kama *Izibongo* ambapo kabla ya utawala wa Wafalme Dingiswayo na Shaka, *umadlekezele!*, taswira zilizotawala zilikuwa za wanyama na wadudu wadogo wasiodhuru kama vile vipepeo na hata nyoka wa mzimu. Kwa ujumla taswira hizi zinajenga picha ya amani na ustawi. Mara baada ya Shaka kuwa mfalme na nchi ya Kwazulu kuteka makoloni ya Natal (1818-1828) na kuitanua himaya ya Wazulu kwa njia ya vita na umwagaji wa damu uliokithiri, taswira nazo zilibadilika katika majigambo ya nyakati hizo. Majigambo yalitawaliwa na taswira zilizojaa damu, na ukatili kuititia usawiri wa maumbo na hali za kutisha kama vile “Simba wa wazulu”, tembo, nyati, chui, nyoka wenye sumu, moto, tufani na hata miti ya miba. Mfalme Shaka aliitwa majina kadhaa ya wanyama na ndege wa kutisha ikiwemo chui, kiboko, na mwewe. Moja ya sifa kuu ya Shaka

¹³ Inasemekana kuwa *Kunguru* weusi huko Zanzibar waliletwa kutoka India au Persia kwa nia ya kula mizoga ya maiti wakati wa utawala wa Sultani. Wanahesabika kwa sasa kuwa ni ndege waharibifu na mikakati ya kuwawinda na kuwatokomeza imeshindikana (<http://sustainableeastafica.org/wp-content/uploads/2013/09/2.-Mazingira-Endelevu-Zanzibar-Bioanuawai.pdf>) na <http://www.zanzibarassembly.go.tz/Hansard/2012/pdf-Octoba-2012/kikao-cha-pili.pdf>). *Taarifa zimesomwa 8/11/2015*

AHMAD KIPACHA

iliyoshadidi katika majigambo ya kumtweza ni ile ya “Ndege alaye ndege wenziwe”. Huo ni msemo wenge mrindimo wa vita vilivypiganwa na Shaka na kuhalikisha maadui zake kiasi cha kuwabeua kwa kuwafananisha na *Izinyoni* au ndege walionaswa katika mtego. (Masango 1996: 67-68, Gisela 1999: 144)

Ngugi wa Thiong'o (1965: 3) naye anatusimulia katika riwaya yake ya *The River Between* kuwa katika nyakati za amani na ustawi, nchi ya Gikuyu, ilitawaliwa na ndege na wanyama walioimba na kuburudisha kwa sauti nzuri na pale hali ilipokuwa si shwari walitoa sauti na mingurumo mikali. Vilevile anatueleza kuwa Wazungu waliitwa “vipepeo” na Wagikuyu na rai ilitolewa na kiongozi wa Wakikuyu aitwaye Chege kuwa wasidhuriwe kabla ya kujua nia na malengo yao kwanza. (Ngugi 1965: 20) Mantiki ni kuwa hakuna sababu ya kuwaangamiza wadudu, ndege au hata wanyama ikiwa hawana madhila kwa ustawi wa jamii husika Katika masimulizi yake, Ngugi anatutanabaisha kuwa amani na ustawi huibua taswira laini za upendo na utulivu na hali ya vita na misukosuko huibua taswira za vitisho na maafa.

Katika kazi za Khamis (2004) na Khatib (2011) ambapo taswira za mapenzi zimetamalaki, ndege watumikao ni wale wasiojenga picha ya vitisho au maafa. Jukumu la “utarishi” wa kukuwadia wapendanao linabebeshwa “Njiwa huuri.”¹⁴ Katika mwimbo uitwao “Mwezi”, Khamis anaonyesha namna watribu mbalimbali huko Zanzibar wanavyomsasambua mwanamke kupitia taswira za mbawa za ndege (2004: 35-37):

Ewe mwezi ewe azizi *nipe mbawa nirukie*,
Ewe mwezi ewe mpenzi *nipe ngazi nipandie*.

Ubei unatupa picha ya “mbawa za kurukia” na “ngazi za kupandia”. Mbawa ni viungo azizi ambavyo wanadamu hatuna katika maumbile yetu na tunawaonea *inda* viumbe wenge navyo na kuzidisha shauku ya kupaa au kukwea juu angani. Viumbe kama majini na mashetani ingawa hatuvioni navyo vinahesabika mawazoni mwetu kuwa na uwezo wa kupaa kwa mbawa: Khamis (keshatajwa: 37) anatunukulia wimbo wa “Shada Langu la Maua” kuwa:

Huvutia mashetani na majini *wenye mbawa*,
Malaika na ruhani wote wamelitambua.

Shada la maua ni taswira ya upendo na mara kadhaa wanawake wamenasibishwa na “ushetani” kwa mintarafu ya Hawa kushawishika kirahisi kula “tunda” kupitia ibilisi. Hakuna taswira ya maafa katika ubeti huo.

Kwa upande wa taswira za vita na maafa, ndege wametumika katika miktadha ya mtu au jamii inapokuwa katika misukosuko kama vile kutawaliwa, kubaguliwa, na kugandamizwa.

¹⁴ Ukuwadi wa njiwa huuri unabainishwa katika beti za Muyaka bin Haji. (Khatib 2011: 201)

Enenda *ndiwa huuri* mwenye cheo cha heshima

Fika ukamuhuburi, haya t'akayokutuma

Dhana ya uhuria inatumika kama kielelezo tu cha sitari pana ya kumsawiri kimpenzi mwanamke.

TASWIRA ZA NDEGE KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

Kundi la *bundi* (*bumu*), *kuku* (*vidoavidoa*), *mumbi*, *kunguru*, *kitati*, *kumbikumbi*, *tai*, *popo kipungu*, *kiku*, *kisiji*, *bata*, *makinda*, *ninga*, *nyuni*, *koti*, *ziku* hutawala katika maandiko au misemo. Msamiati wa *matongotongo* (kupigapiga mbawa), *madege meupe*, *wana wa nyuni*, *ndege manyoya*, *njiwa wa kale*, *nyungo za kurukia na tundu za ndege* inatamalaki katika kazi za *Mashetani* (Hussein 1971), *Al-Inkishafi* (Hichens 1972), *Malenga wa Karne Moja* (1987), *Utendi wa Fumo Lyongo* (Mulokozi 1999) na *Kija: Chungu cha Mwana Mwari wa Giningi* (Kitogo 2005). Kazi hizo zote zinabaini misukosuko na picha ya “vita” katika jamii ya Waswahili na hususani nchi ya Tanzania. Katika *Malenga wa Karne Moja* (Chiraghdin 1987: 54) ndani ya Shairi la “Malumbano” la Suud bin Maamiri (1810-1878) wa Mvita anawajengea wasomaji wake taswira ya “vita” na maafa kupitia, wanyama na ndege “wababe”:

Ai mi! Simba mngwizi, asadi mke mbuwai
Hunyakua kama *kozi*, kwa hila nyingi na rai
Sambe hutendwa ni mbuzi ukamba samba hagwi
Ai *kipanga* na *tai*, nisiyenshiwa ni nyama

Fumo Lyongo naye alikuwa “vitani” na adui zake waliomkusudia kumuangamiza. Anajiita kozi mwenye uwezo wa kuwaangamiza adui zake (nyoka) (angalia Mulokozi 1999: 39).

Katika *Mashetani*, Hussein (1971: 1-2) anatuchorea jamii inayokabiliwa na matabaka na mfumo wa ukoloni mamboleo kupitia kiumbe *shetani* anayejinaki kuwa “mimi siyo jini wala kuhani” bali anauwezo wa kujigeuza “ndege” na kurukia matawini. Kitogo katika *Kija: Chungu cha Mwana Mwari wa Giningi* anaisikitikia jamii yake iliyotumbukia katika uchawi (ufisadi) ambapo maembe (rasilimali) yamekwisha inamiwa na *popo* (mafisadi) yanapopolewa:

Uchawini kuna mwembe dodo *popo* kesha uinamia. (Kitogo 2005: 7)

Robert anajitumbukiza katika kundi la waandishi watumiao taswira za ndege za maafa na misukosuko na si upendo na hali ya utulivu.

Motifu ya Upazo na Ukweli katika Maandiko ya Shaaban Robert

Baina ya mbingu na ardhi ni anga ambalo mwanadamu huhitaji kufanya jitihada kubwa kujijengea uwezo wa kusafiri kati yake. Uwezo wa kusafiri majini na ardhini umefikiwa muda mrefu. Robert anajenga hamasa juu ya uwezekano wa kuvunja mwiko na kumudu kusafiri angani kama ndege:

Wa angani
ndiyo ndege warukao. (Robert 2008: 27)

Amegusia uundwaji wa eropleni katika mipango ya baadaye ya wanadamu, matumizi ya mbawa kwa wakati wake ili kuruka na kupaa kihuria. Rai yake kwa wasomaji wake ni kwamba ingawa

AHMAD KIPACHA

Ndege ndio viumbe vikuu virukavyo, mwanadamu akiongeza juhudhi kidogo lengo hilo litafikiwa. Fikra hizo zimo ndani ya *Kusadikika*:¹⁵

Karibu maisha ya malaika yatafikiwa na watu wa ardhi kama bidii zao zitafululiza hawana mabawa lakini huruka hewani kama ndege kwa vyombo. (Robert 1991b: 47)

Robert anawataka wanajamii wenzake waruke kwa kiwiliwili na kiroho na sio kungojea siku ya kufa ambapo ni roho pekee hupaa na mwili hubaki ardhini. Kupitia watu wa Ardhini katika *Kusadikika* anatoa somo la kukataa:

Kitendo cha kushindwa *kupaa juu mpaka* baada ya mauti; na hivyo, wakaweka bidii ya kuunda chombo ambacho mwendo wake utakuwa katika uongozi wao wenyewe. (Robert 1991b: 42)

Anawarejelea wanajamii wenzake katika riwaya ya *Utubora Mkulima* kupitia miujiza ya kisa cha *Miraji* ambapo Mtume Muhammadi alienda mbinguni kwa msaada wa malaika na farasi mwenye mbawa aitwaye *Buraq* kwa mwili na roho.¹⁶ Mhusika Utubora Mkulima anastaajabu maendeleo yaliyofikiwa kwao Mrima baada ya kutoka vitani nchini Burma na kuishi upagazini kule Uguja akifanya kazi za “kijungu jiko” kwa tajiri wake wa Kiasia.

Alibaini kwamba ile ndoto yake ya ajabu kama ile ya miujiza ya *Miraji* ilikuwa kama darubini ya kuthibitishia kuwako kitu kisichoonekana kwa macho matupu kwa sababu ya udogo au ya kuwa kwa sababu ya kuwa ng’ambo ya upeo wa mwanadamu. (Robert 1968: 18)

Robert anawahimiza wasomaji wake wavunje usemi wa “the sky is the limit”:

Hewa *haina* mpaka
Ndege *huri* huruka. (Robert 1991d: 24)

Kwake fikra na maendeleo hayana ukomo. Ndege yuko huria kuruka atakako sembuse mwanadamu mwenye fikra pana na vipawa lukuki? Anaitia shime hadhira yake juu ya uhuru wa “*kupaa*” na kutawala anga na sayari zinazotuzunguka. Anawapiga shere wasomaji kwa kijembe cha uwezo wa kutembea kwa miguu angani ambapo mhusika wake Utubora katika *Utubora Mkulima* anakuwa sawa na mwanaanga Armstrong aliyetembea mwezini pale alipowazia fursa ya kuanza maisha mapya kwao Mrima na kuwa mkulima. “*Utubora* alijiona kama aliyeokuwa

¹⁵ *Kusadikika* ni riwaya ya kiutopia inayoelezea maisha ya nchi ya angani inayozungukwa na pande nne za dunia, anga na ardhi. Lakini ni nchi inayokabiliwa na ukosefu wa haki za binadamu ambako mhusika mkuu Karama anashtakiwa kwa kuanzisha elimu ya uanasheria. Anajitetea kwa kutoa ushahidi wa siku sita wa dhuluma waliofanyiwa wajumbe sita waliotumwa kupepeleza nchi za jirani na kuleta habari mpya za kimaendeleo na ustawi wa kuigwa. Hukumu inapitishwa baada ya utetezi wa Karama wa hatua ya kufundisha elimu ya uanasheria ili haki itendeke nchini *Kusadikika*.

¹⁶ Katika kisa cha *Miraji* kuna farasi mwenye mbawa aitwae “*Buraq*” na Malaika Jibril. Hizi ni taswira anazo-zirejelea Robert anapoeleza ndoto za Utubora Mkulima na safari za mjumbe wa Mbinguni akijua fika hadhira yake tayari inayo maarifa ya simulizi zake. Kisa cha *Miraji* na taswira zake mbalimbali zimejadiliwa katika Knappert (1966) na Ranne (2010).

TASWIRA ZA NDEGE KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

akitembea kwa miguu angani.” (Robert 1968: 17) Kitendo cha kupata mabadiliko, uhuru na ustawi si ndoto Kwa Robert. Hataki wanajamii wenzake watumie tu hila na misaada “kupaa” kama walivyofanya wajumbe wa Mbinguni na wale wa Ardhini katika riwaya ya *Kusadikika*. Ridhaa mjumbe wa Mbinguni alisaidiwa na Malaika “kusafiri kuelekea mbinguni.” (Robert 1991b: 34) Na ilipotokea haja ya kusafiri kwa mjumbe wa nchi ya Ardhini, aitwaye Amini, hila ya kujifunga pajani kwa ndege mkubwa aiwaye *Mangera* wakati amelala ilitumika:

Amini alishuka katika Ardhi kwa msaada uliopatikana kwa *Mangera*, *ndege wakubwa kabisa* walishao katika Ardhi lakini walalao Kusadikika. (Robert 1991b: 40)

Safari zote mbili ni za kubahatisha na kutotegemewa. *Mangera* ni dege la kutisha halina msaada wowote kwa watu wa *Kusadikika*. Robert anadokeza kuwa kazi yake ni kulala tu *Kusadikika* na kulisha kwo Ardhini. Hivyo madege yaliyopo *Kusadikika* ni wachumia juani na faida kubwa inapelekwa *Ardhini* - kivulini. Tukio la hatari alilolifanya mjumbe Amini lina picha ya kutisha:

Amini alijifunga bila ya kujulikana juu ya paja la *Mangera* aliyekuwa amelala fofofu usiku. Kulipokucha ndege huyo aliamka akaruka mpaka chini. Alitua ziwani. Nusu ya mapaja yake ilikuwa majini. (Robert 1991b: 40)

Umbo la ndege la *Mangera* ni la kuogofya. Si ndege mdogo tuliyemzoea kutuburudisha kwa sauti zake. Ni ndege mwenye uwezo wa hata kumla ndege mwengine. Ndege aliyeuokoa Adili katika *Adili na Nduguze* na yeye pia alikuwa na umbo la kutisha na alitumia miguu aghalabu yenye makucha makubwa kumwokoa Adili aliyeingiwa na hofu kubwa moyoni ya kuwa chakula cha tai, ndege mla mizoga na mwenye kuogofya wanyama, ndege wenziwe na hata mwanadamu. Robert anatuambia:

Palikuja ndege aliyekuwa na umbo la kutisha akamwopoa Adili majini kama koleo; miguu ya ndege ilimshika kwapani akaruka naye. Fikiri wewe mwenyewe hofu aliyoukuwa nayo Adili alijiona ameokoka kuliwa na papa akawa chakula cha tai. (Robert 1980: 34)

Vitisho vinavyoambatana na msaada wa kuopolewa au kupazwa vina taswira ya kuogofya. Jamii ya Waswahili ina visa asili vya “majoka” yanayopazwa kwa minyororo mikubwa kutoka mbinguni huku kukiambatana na wingu zito wakati wa uzukaji wa tukio kama hilo. Shani Kitogo anaelezea namna mhusika *Kija* ndani ya tamthilia ya *Kija*: *Chungu cha Mwana Mwari wa Giningi* anavyojilaumu kuzaliwa na mama yake aliyeingia katika chama cha wachawi (mafisadi) anasema:

Natamani ardhi ipasuke niingie ndani yake, halafu ijiunge tena. Au *mnyororo utoke mbinguni unipaze?* (Kitogo 2005: 36)

Robert anashauri kuwa inapotokea “majoka” yamepea kama ilivyo *Mangera* au mfalme Jeta katika nchi ya Kusini ndani ya *Kusadikika* (Robert 1991b: 23) badala ya kuyapaaza mbinguni anakohadithiya katika *Kusadikika* kuwa kuna halmashauri zenye haki, na kundi la malaika

AHMAD KIPACHA

wema, (Robert 1991b: 36) watu wachukue sheria mkononi. Taswira aitumiayo ni ya mchwa wanaochukuliwa kuwa ni walaji wa rasilimali ya taifa, na anashauri waoteshwe “mabawa” kama kumbikumbi wapeperushwe:

Mchwa ukikaribia kuangamizwa hufanywa kumbikumbi na huoteshwa mabawa mawili. (Robert 1991b: 4)

Ushauri wa Robert kwa wanajamii wenzake wanaokandamizwa na mfumo wa ukoloni na ubaguzi kwa kipindi hicho ni kutumia silaha ya mbawa kuwageuza mchwa kuwa kumbikumbi ili iwe rahisi kuwatokomeza. Taswira ya kuotesha mabawa ina pande mbili zinazokinzana. Kwa upande wa wakandamizaji nao hutumia silaha hiyo hiyo ya kuotesha mabawa wanaharakati na kuzuia kuenea kwa upinzani wa mfumo wao. Katika *Kusadikika* rai inajengwa ya kumzuia Karama asieneze “uzushi” na elimu ya uanasheria; hivyo ushauri unatolewa na Waziri Majivuno kuwa:

Matendo ya mshtakiwa yamekwisha kuwa mabawa ya kutosha kuifanya serikali kufikiri kama yasingepasa kukomesha kabisa kwa mfano uwezao kumzuia mtu mwengine ye yote kuyaigiza.” (Robert 1991b: 4)

Nia na madhumuni ya ombi la Majivuno la kutaka Karama akatwe mabawa ni kumzuia katika safari yake ya kukwea vilele vya ustawi na umaarufu. Robert anaitumia vyema taswira ya uoteshaji au ukataji mabawa katika maandiko yake ili kuibua motifu ya upazo na ukwezi wa kihadhi. Katika *Wasifu wa Siti Binti Saad*,¹⁷ ambapo kuna usambamba wa harakati za Robert na Siti bint Saad za kimaisha, Robert alitumia wino na karatasi pale Siti alipotumia sauti na maungo yake kucheza *nakiti*. Katika kuwaelezea wasomaji wake ubora na mvuto wa sauti ya Siti, Robert hakuwa na zana nyingine ya kutumia isipokuwa taswira ya ndege wadogo waimbao. “Siti aliimba “mchana na usiku kama *kurumbizi*” (Robert 1991c: 16). Ilipobidi Robert kutusimulia namna Siti alivyowapumbaza wasikilizaji wake alipokuwa akirikodi nyimbo zake kule Bombay nchini India, kiasi cha kuwalewesha kwa sauti wasikilizaji wake na hivyo mmoja wa wenziwe aliyetoka naye Unguja kumsihii kwa maneno matatu madogo ya “polepole tuko mbali”, Robert aliona hakuna budi kutumia taswira ya “kuyaotesha mbawa” maneno hayo madogo matatu na kuyapaza juu ya “bahari pana mpaka Afrika ya Mashariki” (Robert 1991c: 46). Robert hakuishia kuelezea msambao wa sauti ya Siti kwa taswira ya uoteshaji mbawa pekee, sauti nyembamba za ndege nazo anazikweza juu angani:

Kwa mbawa zimepambwa,
Kwenda tusikokujua. (Robert 1991d: 9)

¹⁷ *Wasifu wa Siti Binti Saad* ni riwaya ya tawasifu ya muimbaji maarufu wa kike wa taarab kutokea Unguja aliyesadikiwa kuzaliwa mwaka 1880 na kufariki 1950. Robert alipata hidaya ya kuelezea kwa njia ya kumbukumbu maisha ya mwimbaji huyu maarufu na njia za maisha alizozipitia kutokea hali yake duni hadi kuwa maarufu wa kuuza santuri zake duniani kote. Siti ni mfano wa watu duni ambaa Robert amejisawiri naye lakini mwisho wa harakati zake alifaulu kuwa mionganii mwa “watu waliofika kilele cha ustawi” kutohana na kazi na bidii kubwa. (Robert 1991c: 12)

TASWIRA ZA NDEGE KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

Mbali ya habari na sauti kuenezwa au kupazwa kupertia taswira ya kuotesha mbawa, Robert hachoki na mbinu hiyo kuelezea dhana mbalimbali dhahania zisizo na mabawa kwa asili. Katika riwaya ya *Kufikirika*, anayosimulia nchi ya “kufikiria tu” yenye ustawi mkubwa wa rasilimali na uzazi wa watu wake lakini inayokumbwa na mtihani wa mfalme wake na malkia kutobarikiwa kupata mrithi wao kutokana na utasa, shughuli zote za kimaisha zinasimamishwa na kila jitihada, ujuzi na maarifa ya nchi yanatumika kuhakikisha Mfalme anapata mtoto. Habari za malkia wa *Kufikirika* kushika ujauzito zinaotesha “mbawa” na watumishi wake wa ndani:

Habari ilinong’onwa na watumishi wachache katika nyumba ya mfalme kuwa Malkia alikuwa ana mimba. Habari hiyo *iliota mbawa* ikaenea katika nchi nzima. Mwaka haukulizika akazaliwa mtoto wa kiume. (Robert 1991a: 17)

Robert alikuwa na hiari ya kusimulia habari hiyo kwa lugha ya kawaida tu ya kuwa habari ilisambaa, lakini aliona umuhimu wa kuturejelesha katika taswira ya kuota mbawa kuelezea kuwa hata habari nayo inaweza kupaa kama ndege. Somo la kuotesha mbawa haliishii katika habari pekee, maneno “katika hewa hupaa” (Robert 1991d: 9) na wakati unashimuliwa kiontolojia kuwa una “*mabawa* kama ndege” (Robert 1991b: 10). Ukata baada ya ukwasi wa mali hubainishwa kwa nahau ya “*kuota mbawa*” (Robert 1991d: 20). Na “tabia” ya mtu nayo inapambwa kwa taswira ya mbawa:

Tabia kitu cha mauzauza, ilikuwa *pandio* au *mbawa* kubwa za mtu (Robert 1991c: 53).

Robert anatugusia hapa juu ya *mbawa* kuwa ni *pandio* au zana ya upazo na ukwezi. Robert anawasaidia wasomaji wake kuelezea dhana zake za kipando au ngazi kwa sura pale anapounda lakabu ya “Hunde alikuwa Waziri wa ngazi” (Robert 1980: 35)¹⁸ na katika *Adili na Nduguze* anawatanabaisha wasomaji wake juu ya *milango* (ya ufahamu na elimu) na “upandaji wa vidato”. Adili anapitishwa na Robert kupertia mlango mdogo na mara tu:

Alipopanda vidato vichache, kwanza alikuwa akipanda kwa kusitasita. Lakini sasa dalili zile zilimvuta akafululiza kupanda. Aliendelea mpaka orofani... Akafunua pazia. Alipofanya hivyo macho yake yalionna mlango wa tarabe. (Robert 1980: 25)

Kipando cha vidato au ukweaji kileleni hadi “ghorofani” na dhana ya “*milango*” na “pazia” ni ishara ya kukwea vilima vya hadhi na kuongeza maarifa zaidi, haswa kielimu. Robert anasisitiza juu ya safari ya kukwea ngazi kutoka katika unyonge hadi ustawi wa watu wake na yeye mwenyewe akiwa katikati ya harakati hizo. Wahusika wake kama vile mwalimu wa mtoto wa mfalme katika *Kufikirika* anaonyeshwa kuwa ni mfano wa kukwea hadhi ambapo mtoto wa mfalme anamsifu Mwalimu wake huyo wa zamani aliyemjengea msingi imara wa maarifa:

¹⁸ Usawiri wa lakabu za Robert katika maandiko yake umejadiliwa kwa kina na Ngonyani (2001).

AHMAD KIPACHA

Kutoka maisha ya desturi uliingia katika utabiri. Kisha ukaenda katika ualimu. Halafu ukaingia katika ukulima. Na Kutoka katika ukulima ultumbukia katika gereza kungoja kuchinjwa kwa kafara, na baadaye kuwa waziri. (Robert 1991a: 49)

Robert anajenga hoja pana kuwa yeze na watu wa taifa lake la Tanganyika wamo katika “kupanda ngazi... kama kila taifa jengine.” (Robert 2008: 1-2)¹⁹ Hivyo jitihada ndio ufunguo wa mafanikio.

Wako walioanza maisha katika unyonge na dhararu wakapanda mpaka juu ya kilele cha heshima na utukufu. (Robert 1980: 43)

Siti binti Saad katika *Wasifu wa Siti binti Saad* alichoshwa na “utawa” na hali duni ya kijijini kwao Fumba ya uchuuzi wa vyungu; kwa hiyo, “alitoka ufichoni na kuja mjini na alipata maendeleo na ustawi mkubwa.” (Robert 1991c: 25) Hakutaka kufumbatwa na mfumo “ulioviza fikira, akili, adili na bidii.” (Robert 1991c: 27) Robert anaionya hadhira yake juu ya tabia ya kuwadharau watu wengineo. Anaonya kwamba tabia hiyo haijengi kwani:

Ukidunisha mtu leo utamwona juu ya kilele cha utukufu kesho. (Robert 1991c: 23)

Robert anajipambanua yeze kama sauti na mtetezi wa wanyonge waliodunishwa na ambao wanataka kujinasua katika hali hiyo kwa kukwea ngazi za ustawi na utukufu hapa duniani kama alivyo kiumbe ndege.

Robert anaelewa fika juu ya taswira ya “kukatwa mbawa” na madhara ya kushushwa hadhi, kubaguliwa na kukumbwa na umasikini uliotopea. Safari au njia hiyo ameipitia yeze mwenyewe na familia yake. Katika riwaya yake ya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*,²⁰ anasafiri na familia yake kutoka Tanga hadi Mpwapwa ambapo alistahiki hadhi ya abiria daraja la pili, lakini aliposhushwa na familia yake na kulazimishwa kupanda lori (Robert 1991d: 53) kuwapisha abiria wenye asili ya kiasia wachukue nafasi yake na kuachwa akipigwa baridi na familia yake mara baada ya kufika alfajiri Mpwapwa ili kuanza kazi ya serikali, kulimgutusha juu ya hadhi yake duni. Kitendo hicho hakina tafsiri nyingine zaidi ya “kukatwa mbawa.”²¹ Kwa kudhihiri nafasi yake na wanajamii wenzake anawagutusha wanajamii wenzake kuwa wao ni ndege walio

¹⁹ Hussein (1971: viii) katika *Mashetani* anajenga taswira ya upandaji na ushukaji ngazi kimatabaka kutokana mifumo inayokinanza kuititia wahusika Kitaru na Juma: “Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mikono”.

²⁰ Katika riwaya hii Robert anaelezea kishajara maisha yake, familia yake, ajira, huzuni na furaha, na vipawa vyake vya uandishi. Mtu anapokatwa mbawa anakuwa ananyimwa fursa na kukatizwa ndoto zake. Anadumazwa na kutopandishwa ngazi. Robert anagundua kuwa rangi yake na Waafrika watatu pale katika idara ya Wanyama ambako alikuwa anafanya kazi ilikuwa kitambulisho cha hadhi yao ya daraja la tatu.

²¹ Methali ya Kimwera inasema *Nnateme ndegule lipapiko* “usimvunje bawa ndegule” ikimaanisha kuwa ndege aitwaye ndegule huonyesha warina asali miti mikubwa ambamo nyuki aghalabu hutengeneza asali ndani ya mapango yake. Unapomvunja bawa ndege aina ya ndegule unakuwa umejitia hasara mwenyewe. (Mbilla 2002: 44) Robert pia ametumia taswira ya vidudu mbawa aina nyuki kwa kuwatofautisha *nyuki asali* na *nyuki wavivu* katika *Utubora Mkulima*. (Robert 1968: 34)

TASWIRA ZA NDEGE KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

katika hatari na misukosuko ya kuwindwa muda wote. Anawataka wasijisahau na wawe kama “Ndege waliostuliwa na mshindo wa kumbweye.” (Robert 2008: 93)

Kumbweye ni kifaa au silaha inayotumika kuwatimulia ndege waharibifu mashambani. Kwa vile wao ni ndege wema maadui zao wana silaha za kumbweye za kuwaangamiza. Silaha hizo ni pamoja na ukosefu wa elimu, haki, ubaguzi, na umasikini. Anawashauri nao watumie kumbweye hiyo hiyo kujikwamua katika unyonge unaowakabili. Badala ya kumbweye yenyе mawe ndani yake watumie yenyе sauti kali yenyе madhara makubwa itumiayo silabi tatu yaani u-hu-ru! Kilio cha uhuru anakielezea katika riwaya ya *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* kuwa ni:

Kumbweye ya kutafuta suluhihisho kwa kutumia sauti kali yenyе silabi tatu: u-hu-ru.
(Robert 1991d: 116)

Robert anawajengea wanajamii wenzake moyo wa ujasiri kwa kuwaadhi kuwa wasione kuwa maneno hayo madogo ya silabi tatu ya u-hu-ru ni madogo. Anawakumbusha kuwa “ufunguo mdogo hufungua kufuli kubwa.” (Robert 1968: 12)

Unapokuwa katika misukosuko maliwazo ni tunu adhimu. Robert, kwa kuyatambua hayo, anarejelea tena katika taswira ya ndege, na safari hii anaililia nchi yake ya Tanganyika ambayo ni kimbilio lake na kuamua kuiita kwa taswira ya “kiota” cha ndege. Sifa ya kiota cha ndege anaisawiri katika shairi la “Tanganyika” ndani ya *Diwani ya Shaaban 10* (2) kuwa:

Wewe ni *kiota* changu, siku ya giza na mvua.
Na dhoruba na mawingu, na msongano wa hewa.

Taswira ya kiota cha ndege inachorwa kwa wasomaji wake kama mahali pa mapumziko. Robert anajenga rai ya “kila mtu kwao ni kivulini na ugenini ni juani” (Robert 1980: 14). Mabadiliko ya kiutawala na ukandamizaji si hoja ya kukikimbia kiota chake. Matumaini yake ni kuwa kiota cha “wenyeji wa Afrika, wana Tanganyika hakina budi kiwe na ustawi na amani:

Ndege wa manyoya hupatana katika *kiota* chao kidogo.” (Robert 1991d: 66)

Waafrika na wanyonge ni ndege wa manyoya²² ambao hawana budi kuwa na umoja na maele-wano katika kujitafutia ustawi wao.

Robert anajipigia mfano yeye mwenyewe na kujinaki kifua mbele kuwa hatashikwa na *mkunguru* (homa au uoga) kwa vile analiwazwa na “sauti za membe na vitwitwi” (Robert 2008: 51). Membe na vitwitwi ni videge vidogo vyenye sauti nyororo na sio sauti kali za kuogofya kama zilivyo za Mangera na majitu makubwa kama vile *Mrefu*. Hata hivyo si kila sauti ya ndege wadogo ni kiliwazo. Robert alipobahatika kusafiri kiuhalisia kwenda Unguja kwa ajili ya

²² Hussein (1971: 48-49) anajenga taswira ya manyoya kama tabia ya ubadhirifu kuititia Kitaru. Anasema kuwa kila mtu na kitu kimeota manyoya na kila yakinyonyolewa yanarudi tena. Na Kitogo (2005: 5) anashadidua kuwa “sitakufa kama mbega anayejinyonyoa manyoya yake. Manyoya yangu yatabaki duniani yakipamba midomo ya walimwengu kwa uzuri wangu.”

AHMAD KIPACHA

kumzuru na kumhoji Siti binti Saad ili kuandika wasifu wake alimkuta yu mgonjwa kitandani. Robert alirejelea tena katika taswira za ndege kuwahadithia wasomaji wake kuwa alizipokea habari za ugonjwa wa Siti bint Saad mithili ya kumsikia “bundi” aashiriaye vifo:

Habari ile haikunipa tamaa ya kumwona. Nilianza kushuku kwamba ilikuwa *ndege mbaya kwangu*. (Robert 1991c: Utangulizi)

Fungu la ndege wabaya wanaowakilisha wakandamizaji na maadui wa ustawi halifichwi na Robert. Katika *Siku ya Watenzi Wote* ambapo Robert anaipigania Jumuia ya Adili na umoja wa itikadi katika nchi yake ya Tanganyika iliyoanza kuonja utamu wa kujitawala, bado anaona kuwa kuna baadhi ya watu amba ni sawa na “ndege wabaya”. Baadhi ya watu hao wachache wanatoka katika kundi la wanaitikadi na wafuasi wao amba amewafananisha na “*ndege fulani wasifiao kichaka* usiku kwa vile kimewahifadhi lakini hukilaani mara kunapopambazuka.” (Robert 2008: 7) Kwa Robert maumbile na mabadliko ya hali ya nchi yake ya Tanganyika hayamfanyi atake kutoroka na kuikimbia nchi yake bali ni kichochea cha kutimiza wajibu wake kama mtetezi wa wanyonge.

Motifu ya Safari ndani ya Taswira za Ndege za Robert

Dhana ya “safari” inatafsiriwa katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004: 355) kuwa ni “tendo la mtu kwenda mahali fulani ambapo ni mbali na pale alipo”. Tunamwona Shaaban Robert akiliombea dua shairi lake la “Mgeni Wetu” katika *Mwfrika Aimba* “liote mbawa”, liruke, lisafiri na kuenea “mbali na pale alipo” na lisambae dunia nzima kupitia shairi:

Mungu lioteshe mbawa,
Liruke na kusafiri,
Lienee na dunia. (Robert 1969: 30)

Kuota mbawa kama ndege ni ishara ya safari. Kwa kumtumia kiumbe ndege, Robert katufumba kuwa “*Ndege mwenye kutua tawini lazima aruke.*” (Robert 1991d: 48) Nini hasa maana yake? Iwapo ndege atabaki tawini ataishije? Lazima aruke kutafuta ustawi. Bado Robert anatufumba zaidi katika *Kufikirika* kwamba “maisha ni ndege asiyerudi mahali aliporuka.” (Robert 1991a: 42) Hii inamaanisha maisha ni safari (ndege) sawa na moshi. Katika *Adili na Nduguze* anatujengea rai kuwa “maisha ni safari na dunia ni matembezi kwa wanadamu.” (Robert 1980: 10) Kwa mantiki ya kianalojia sitiari ya kuwa maisha ni safari ni sawa na kusema maisha ni ndege.

Katika safari kuna mwanzo, katikati na mwisho wa safari. Siti alipotoka kwao Fumba hadi Unguja ni mwanzo wa safari; kushindwa kwake kuimba kwa mara ya kwanza na kubezwa na wapinzani wake ni vikwamo vya njiani. Kufanikiwa kusafiri hadi Bara Hindi, na santuri zake kuuzwa dunia nzima ni upeo wa safari yake. Sambamba na Siti, Robert anatueleza katika *Siku ya Watenzi Wote* kuwa anawaaga buriani wasomaji wake:

TASWIRA ZA NDEGE KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

Chombo changu kimekwenda safari ndefu sana; nacho kinakaribia *bandari* sasa. Nina maarifa ya miaka ya *msukosuko na ya taabu* ya kuniongoza. Yaliyokuwa maafa kwangu yamekuwa *dira* yangu. Huna budi kungoja zamu yako na ukumbuke akili nzuri ya mwepuko ambayo tumetunukiwa kuwa kama hadhari ya uovu, si jambo la kudharauliwa wala kutupiliwa ovyo. (Robert 2008: 92)

Robert anatuchorea vipengele kadhaa vikuu vya safari; yeye kama *abiria, vyombo, dira, bandari*. Hii ni njia ya majini ambayo ni sawa na ile ya angani na ardhini. Taswira anayotujengea ni kuwa yuko ukingoni mwa safari yake. Kiujumla Robert na wahusika wake walisafiri katika njia mbili kuu: safari za kufikirika mawazoni na zile za kiuhalisia au pale nyayo zake zilipofika. Katika safari zake halisi ambapo nyayo zake ziligusa zilitegemea vyombo vya kuundwa kama motokaa, lori, na meli; kamwe hakupata nafasi kuonja uhondo wa “ndege-ulaya” au eropleni. Robert katika maandiko yake anaonekana akizuru kifikra pande zote nne za dunia, yaani nchi za Kaskazini (Ulaya), Mashariki (Uasia), Magharibi (Amerika?) na Kusini.

Pia, tunamwona akisafiri kwa msaada wa Malaika (mwenye mabawa) kwenda nchi ya Mbinguni. Vilevile, amethubutu kwa hila kumtumia ndege “Mangera” kusafiri hadi Ardhini. Katika *Utubora Mkulima* Robert anasafiri kifikra hadi vitani. Pia, anatembelea jiji la London, Edinbrugh na makumbusho ya Bernard Shaw, vyuo vya Oxford na Cambridge katika *Kielezo cha Insha*. Na kama mwanadamu mwengine, matembezi yake yana mwisho wake ila rai yake ni kuona jina lake linadumu. Ndiyo maana anasisitiza kuwa “Mtu huhesabiwa kwa matendo na sio umri.” (Robert 1991c: 49)

Kwa mwamvuli wa Siti, anajisemea kuwa “moyo wa Siti ulikuwa na kiu ya nchi ngeni... nyayo zake zilikuwa na mwasho wa safari” za ndani na nje. (Robert 1991c: 45) Robert alipozuiwa kusafiri kwa nyayo zake alitumia mbawa kupaa kifikra na kwenda atakapo. Rai yake kuu ni kuwa kama alivyo Siti na kipawa cha sauti, alichokuzwa na “watrib” mashuhuri nchini na duniani, naye alikuwa na kipawa cha uandishi, ambavyo vyote vilihitajika “kukuzwa” na “kupali-liwa.” (Robert 1991c: 8) Katika kusafiri au kupaa kuna faida nyingi. Mojawapo ni “ufunguaji wa fikira ngeni katika ubongo” wake (Robert 1991b: 1) kwa vile “mti hauendi bila nyenzo.” (Robert 1991c: 41) Faida nyingine ni kuthibitisha aliyyasikia na kuyasoma kwa macho. Adili alithibitisha masimulizi ya ndugu zake juu ya faida za safari zao.

Adili aliambiwa sifa za nchi ngeni... ndugu zake ...walimvuta Adili kusafiri pamoja nao kwa sababu faida ya safari ...ni pamoja na kupata elimu mpya, kuelewa tabia za watu mbalimbali na kukutana na marafiki wa kweli... (Robert 1980: 16)

Robert anatudokeza kuwa anatamani jina lake liingizwe katika kundi la akina Mwanakupuna, Muyaka Bin Haji, Sheikh Amri Abeid au Bernard Shaw baada ya kumaliza “matembezi” yake hapa duniani na roho yake “kupaa” na kukwea hadhi na sifa mustajaba katika mabustani ya mbinguni au “Jumuiya ya Adili,” yaani jamii ya usawa, uhuru na haki.

Hitimisho

Dunia ya Shaaban Robert imezungukwa na mazingira ya wenyiji Waafrika kuwa chini ya milki ya wageni huku ubaguzi, kunyimwa haki, kunyonywa na kukosa maendeleo kukitamalaki. Robert anaitumia taswira ya ndege na mbawa zake kutujengea rai ya kupaa, kukwea hadhi na kusafiri katika harakati za kutafuta ustawi wa kimaisha. Robert anaitaka hadhira yake izinduke na “kusafiri” kiuhalisia na kifikra katika mwili na roho. Hitimisho letu ni kuwa Robert kafafulu kutumia taswira za ndege wa kutisha na kuogofya kuwajengea wasomaji wake picha ya kani-kinzani zinazomkumba ye ye na wanajamii wenzake. Kupitia motifu ya upazo, ukwezi na safari za kimaisha, Robert anajipambanua kama mwandishi stadi wa ujenzi wa taswira. Mchango wetu mdogo katika makala haya ni kujaribu kufumbua fumbo la mahusiano baina ya taswira za ndege na “safari” zake za *kifikra* na zile *halisi* katika duru nzima ya “kipopo” cha usafiri wa kimaisha wa gwiji huyu wa utunzi hapa duniani.

Marejeleo

- Armstrong, Edward. 1958. *The Folklore of Birds: An Inquiry into the Origin and Distribution of some Magico-Religious Traditions*. London, England: Collins Inc.
- Asante Eric, Kyuofu Steve, & Larbi, Stephen. 2015. The Symbolic Significance of motifs on selected Asante religion Temples. *Journal of Aesthetics & Culture* 7: 1-11.
- Chiraghdin, Shihabdin (mh). 1987. *Malenga wa Karne Moja*. Nairobi: Longman.
- Gibbe, Abel. 1978. *Shaaban Robert Mshairi*. Dar es Salaam: TUKI.
- Gisela, Feurle. 1999. Shaka and the Changing Perspectives Teaching South African Literature and History at a German College. *Alternation* 6, 2: 134-149.
- González, Susana. 2000. Broken Wings of Freedom: Bird Imagery in Toni Morrison’s novels. *Revista de Estudios Norteamericanos* 7: 75-84.
- Harries, Lyndon. 1966. Tales from Tanga. *East African Journal* 3, 2: 4-5.
- Harries, Lyndon. 1975. Shaaban Robert: Man of Letters, *Présence Africaine* 93: 194-199.
- Hichens, William. (ed) 1972. *Al-Inkishafi: The Soul’s Awakening: Sayyed Abdallah Nasir*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hussein, Ebrahim. 1971. *Mashetani*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Khamis, Said. 2001. Classicism in Shaaban Robert's Utopian Novel, ‘Kusadikika’. *Research in African Literatures* 32, 1: 47-65.

TASWIRA ZA NDEGE KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

- Khamis, Said. 2004. Images of Love in Swahili Taarab Lyric: Local Aspects and Global Influence. *Nordic Journal of African Studies* 13, 1: 30-64.
- Khatib, Muhammed. 2011. *Chanjo za Matakwa ya Mwanamume katika Mwili wa Mwanamke: Ulinganisho wa Ushairi wa Muyaka Bin Haji na Shaaban Robert*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Kitogo, Shani. 2005. *Kija: Chungu cha Mwana Mwari wa Giningi*. Dar es salaam: TUKI.
- Kipacha, Ahmad. 2015. The Blason Populaire in Swahili Paremia. *Proverbium* 32: 205-220.
- Knappert, Jan. 1966. Miiraji – The Swahili Legend of Mohammed's Ascension. *Swahili* 36, 2: 105-156.
- Lutwack, Leonard. 1917. *Birds in Literature*. Florida: University Press of Florida.
- Masango, Elvis Mphephethi. 1996. *Imagery in Traditional and Modern Praise Poetry in Zulu*. Unpublished MA Dissertation. Rand Afrikaans University.
- Mbillia, J. K. 2002. *Methali za Kimwera*. Ndanda: Benedictine Publications Ndanda.
- Mlingwa, Charles & Kiango, John. 2006. *Kamusi ya Ndege kwa Picha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mnenuka, Angelus. 2010. Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Fleva: Mifano kutoka katika Nyimbo Teule. *Mulika* 29 & 30: 69-93.
- Moreman, Christopher. 2014. On the Relationship between Birds and Spirits of the Dead. *Society and Animals*: 1-22.
- Mulokozi, Mugyabuso. (mh) 1999. *Tenzi Tatoo za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, Mugyabuso. (mh) 2002. *Barua za Shaaban Robert (1931-1958)*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, Mugyabuso & Kitogo, Shani. (wah) 2007. *Mithali na Mifano ya Kiswahili: Shaaban Robert*. Dar es Salaam: TUKI.
- Ndulute, Clement. 1987. Shaaban Robert's Poetic Landscape: From Ethnicism to Nationalism'. *Kiswahili Juzuu* 54: 92-116.
- Ngonyani, Deo. 2001. Onomastic Devices in Shaaban Robert's Narratives. *Journal of African Cultural Studies* 14, 2: 125-136.
- Oriedo, Hannington. 2000. *Fani katika Riwaya za Shaaban Robert: Kusadikika, Utubora mkulima na Siku ya Watenzi wote. Uhakiki wa Kiurasmikanuni*. DPhil ambayo haijachapishwa. Moi University.

AHMAD KIPACHA

- Ponera, Athumani. 2014. *Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi*. Tasnifu ya Uzamivu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Razaq, Abdur. 2011. Symbolic Significance of Bird in Thomas Hardy's The Mayor of Casterbridge. *The Dialogue VI*, 2: 187-195.
- Ranne, Katrina. 2010. Heavenly Drops the Image of Water in Traditional Islamic Swahili Poetry. *Swahili Forum* 17: 58-81.
- Robert, Shaaban. 1954. *Kielezo cha Insha*. Johannesburg: Witwatersrand University Press.
- Robert, Shaaban. 1968. *Utubora Mkulima*. Nairobi: Evans Brothers Limited.
- Robert, Shaaban. 1969. *Mwafrika Aimba*. Nairobi: Nelson.
- Robert, Shaaban. 1973. *Kielezo cha Fasili*. Nairobi: Nelson.
- Robert, Shaaban. 1980. *Adili na Nduguze*. Dar es salaam Tanzania Publishing House.
- Robert, Shaaban. 1991a. *Kufikirika*. Dar es salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Robert, Shaaban. 1991b. *Kusadikika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Robert, Shaaban. 1991c. *Sinti Binti Saad*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Robert, Shaaban. 1991d. *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Robert, Shaaban. 2008. *Siku ya Watenzi Wote*. Dar es Salaam: TUKI.
- Rowland, Beryl. 1978. *Birds with Human Souls*. TN: University of Tennessee Press.
- Seeman, Erik. 2010. Reassessing the 'Sankofa Symbol' in New York's African Burial Ground. *William and Mary Quarterly* 67: 101-22.
- Sengo, Tigit. 1975. *Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi Yake*. Nairobi: Litho Limited.
- Senkoro, F.E.M.K. 1988. *Ushairi Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Thomas, Yunus. 2015. *Usawiri wa Mbinu ya Metonomia Katika Riwaya za Shabaan Robert: Uchambuzi wa Kufikirika na Kusadikika*. Tasnifu ya MA Kiswahili ambayo haijachapishwa. Tumaini University Makumira.
- TUKI. 2001. *Kamus ya Kiswahili Kingereza-Swahili English Dictionary*. Dar es salaam: TUKI
- wa Thiong'o, Ngugi. 1965. *The River Between*. London: Heinemann.

TASWIRA ZA NDEGE KATIKA MAANDIKO YA SHAABAN ROBERT

- Wamitila, Kyallo M. 2003. *Kamus Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books Limited.
- Yahaya-Othman, Saida & Abdulhakim, Yahya (wah) 2004. *Hewani Mwana Hewani: Tenzi za Zaynab Himid Mohamed*. Dar es Salaam: TUKI.
- Zhukov, Andrei. 1998. Shaaban Robert in the Russian Language. *Swahili Forum* 5: 185-189.